# Ripoti ya Uwajibikaji

## Serikali Kuu

**2016-17**



# Ripoti ya Uwajibikaji

## Serikali Kuu

## 2016-17

Kwa kushirikiana na:
Mpango wa Usimamizi Bora wa Mapato ya Umma
(Good Financial Governance)

Unaotekelezwa na:

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Kwa niaba ya:

Co-funded by European Union

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development
and Cooperation SDC

# Yaliyomo

Orodha ya Vifupisho ........ ii

Dibaji ........ iii

**Sehemu ya Kwanza**

Hati za Ukaguzi ........ 1

Aina ya Hati zitolewazo na CAG ........ 1

Mwenendo wa hati za ukaguzi ........ 2

**Sehemu ya Pili**

Utekelezaji wa Mapendekezo ya miaka iliyopita ........ 3

Mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo ya CAG ........ 3

Mwenendo wa utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ........ 3

**Sehemu ya Tatu**

Mambo Muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa 2016/17 ........ 4

Jambo la 1: Utekelezaji wa Bajeti ya Taifa Usioridhisha ........ 4

Jambo la 2: Changamoto Katika Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi ........ 6

Jambo la 3: Mapungufu Katika Usimamizi wa Deni la Taifa ........ 7

Jambo la 4: Rasilimali za Umma Zinavyoathiriwa na Udhaifu wa Udhibiti wa Mifumo ya Ndani ........ 8

Jambo la 5: Madhara ya Uhaba wa Watumishi ........ 9

Jambo la 6: Wakala wa Serikali Bado ni Tegemezi kwa Serikali Kuu ........ 10

Jambo la 7: Vyama vya Siasa Kutozingatia Sheria za Fedha ........ 11

**Sehemu ya Nne**

Hitimisho ........ 12

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| **WAJIBU** | WAJIBU - Institute of Public Accountability |
| **CAG** | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **GIZ** | Shirika la Maendeleo la Ujerumani |
| **NBAA** | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu |
| **IPSASs** | Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma |
| **PAC** | Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu |
| **EFD** | Mashine ya Kielektroniki ya kukusanya Mapato |
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |

# Dibaji




WAJIBU ni taasisi fikra ya uwajibikaji wa Umma iliyoanzishwa mwaka 2015 kwa lengo la kukuza mazingira ya uwajibikaji na utawala bora hapa nchini. Ili kukamilisha adhma hiyo, WAJIBU kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2016/17 ya Serikali Kuu, imeandaa Ripoti ya Uwajibikaji katika Serikali Kuu. Serikali Kuu kisheria inajumuisha Wizara, Wakala, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Balozi.

Katika kuandaa ripoti hii, WAJIBU imeshirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) nchini Tanzania kupitia Mpango wa Usimamizi Bora wa Mapato ya Umma (*Good Financial Governance*). Mpango huu unatekelezwa na GIZ kwa niaba ya Umoja wa Ulaya, Serikali ya Ujerumani na Shirika la Maendeleo la Uswisi.

Ripoti hii inajumuisha mambo yenye umuhimu mkubwa kwa jamii (High public interest issues) yaliyoibuliwa na CAG kwa mwaka 2016/17 katika ukaguzi wa Taasisi 237 sawa na asilimia 98 ya taasisi 241 zilizotakiwa kukaguliwa. Taasisi 4 kati ya taasisi 237 zilizokaguliwa hazikuweza kupata hati ya Ukaguzi kwa sababu ndio tu zilikua zimeanzishwa. Pia, ripoti hii imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na CAG katika ukaguzi wa Serikali Kuu yenye umuhimu mkubwa kwa jamii. **Madhumuni ya mapendekezo ya CAG ni kuongeza tija, ufanisi, uwajibikaji na utawala bora katika usimamizi wa makusanyo na matumizi ya rasilimali za umma**. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa kwa Maafisa Masuuli kutekeleza mapendekezo hayo. Ripoti hii inaweza kutumika kama; nyenzo ya kufundishia wadau mbalimbali, chanzo cha taarifa katika kuandaa machapisho mbalimbali ya kuelimisha umma au kusambazwa kwa wadau wengine.

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu nne (4); sehemu ya kwanza ni hati za ukaguzi, sehemu ya pili ni utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, sehemu ya tatu ni mambo muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa mwaka 2016/17 na sehemu ya nne ni hitimisho.

WAJIBU inawakaribisha kuisoma ripoti hii na kutoa maoni yatakayochangia kuboresha ripoti zitakazofuata.




Ludovick S.L. Utouh
**Mkurugenzi Mtendaji**
**WAJIBU – Institute of Public Accountability**

# Sehemu ya Kwanza

## Hati za Ukaguzi

Hati za Ukaguzi ni maoni ya Mkaguzi wa Hesabu kuhusu hesabu za Taasisi iliyokaguliwa. Maoni haya yanaonesha kama hesabu zilizokaguliwa zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kihasibu vya kimataifa (IPSASs) na matamko yanayotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA).

## Aina ya Hati zitolewazo na CAG





**Katika ukaguzi wa sekta ya umma, wakaguzi hutoa kati ya hati zifuatazo;**


- **Hati Inayoridhisha:-** Hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu.
- **Hati Yenye Shaka:** - Hesabu zinakuwa na makosa ya msingi ya kiuhasibu yanayohusu mapato, matumizi au rasilimali za taasisi.
- **Hati Isiyoridhisha: -** Hesabu na rasilimali kwa kiasi kikubwa zina makosa ya msingi ya kiuhasibu na kiutendaji pamoja na usimamizi mbovu wa mifumo ya udhibiti ya ndani.
- **Hati Mbaya (Kushindwa kutoa Hati): -** Tamko la mkaguzi pale ambapo mkaguliwa hana kumbukumbu za fedha na rasilimali zinazotosheleza kutayarisha mahesabu ya taasisi yaliyo sahihi pamoja na kuwepo udhaifu mkubwa wa usimamizi wa mifumo ya udhibiti ya ndani

## Mwenendo Wa Hati za Ukaguzi

Katika ukaguzi wa mwaka 2016/17, kati ya taasisi 241 zilizokaguliwa, CAG alitoa hati kwa taasisi 237 ambazo zinajumuisha Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Balozi, Bodi za Mabonde ya Maji, Vyama vya Siasa na Mifuko Maalum ya Fedha. Kati ya taasisi 237 zilizotolewa hati za ukaguzi, taasisi 204 sawa na asilimia 86 zilipata Hati Zinazoridhisha; taasisi 22 sawa na asilimia 9 zilipata Hati Zenye Shaka; taasisi 4 sawa na asilimia 2 zilipata Hati Zisizoridhisha na taasisi 7 sawa na asilimia 3 zilipata Hati Mbaya. Taasisi zilizopata Hati Zisizoridhisha ni; Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania; Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (Hombolo); Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori na Hesabu Jumuifu za Serikali. Hati Mbaya zote 7 zilitolewa kwa vyama vya siasa kama ifuatavyo; Chama cha Alliance for Tanzania Farmers, Chama cha Kijamii, Chama cha Sauti ya Umma, Chama cha Tanzania Democratic Alliance, Chama cha Tanzania Labour Party, Demokrasia Makini na Chama cha National League for Democracy. Mwenendo wa hati za ukaguzi katika Serikali Kuu kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1 hapo chini.

### Kielelezo Na .1 : Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Serikali Kuu mwaka 2014/15 hadi 2016/17



# Sehemu ya Pili

### Utekelezaji wa Mapendekezo ya miaka iliyopita


Sehemu hii inazungumzia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG pamoja na maagizo ya Kamati ya Usimamizi ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) ya miaka iliyopita.

### Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG

Katika mwaka 2015/16, CAG alitoa jumla ya mapendekezo 85 katika ukaguzi wa Serikali Kuu. Kati ya mapendekezo hayo, mapendekezo 14 sawa na asilimia 17 yametekelezwa, mapendekezo 51 sawa na asilimia 60 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji, mapendekezo 9 sawa na asilimia 10 hayakutekelezwa na mapendekezo 11 sawa na asilimia 13 hayakutekelezwa kwa kuwa yalikuwa yamepitwa na wakati.

Hivyo, kutokana na uchambuzi huu utekelezaji wa mapendekezo ya CAG bado ni mdogo ukilinganisha na utekelezaji wa Mapendekezo ya mwaka 2014/15 ambayo yalitekelezwa kwa asilimia 19.

### Kielelezo Na. 2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG kwa mwaka 2016/17




### Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Katika kupitia ripoti za ukaguzi za taasisi mojamoja, Kamati ya Kudumu ya Usimamizi ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilitoa maagizo 16 ambayo yalihitaji utekelezaji wa Serikali kupitia kwa Maofisa Masuuli wa taasisi husika. Kati ya maagizo hayo, ni agizo 1 sawa na asilimia 6 tu lililotekelezwa, maagizo 10 sawa na asilimia 63 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji, maagizo 3 sawa na asilimia 19 hayakutekelezwa na maagizo 2 sawa na asilimia 12 hayakutekelezwa kwa kuwa yamepitwa na wakati.

# Sehemu ya Tatu

## Mambo Muhimu Yaliyojitokeza Katika Ukaguzi wa Mwaka 2016/17

Sehemu hii ya ripoti inahusu uchambuzi wa mapungufu yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wa taasisi zilizo chini ya Serikali Kuu kwa mwaka 2016/17, ikiwa ni pamoja na kuonesha athari zinazoweza kutokea kwa jamii endapo mapendekezo hayo hayatatekelezwa. Pia, sehemu hii inashauri nini kifanyike ili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa katika ripoti ya CAG kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa. WAJIBU imefanya uchambuzi wa mambo muhimu 7 yaliyojitokeza kama ifuatavyo.

### Jambo la 1: Utekelezaji wa Bajeti ya Taifa Usioridhisha

Katika mwaka 2016/17, Serikali iliidhinisha bajeti ya Taifa ya Sh. 29.55 trilioni ikiwa ni ongezeko la Sh. 7.05 trilioni sawa na asilimia 31.35 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/16 ambayo ilikuwa ni Sh. 22.50 trilioni.

Vyanzo vya mapato vilivyoainishwa ni pamoja na mapato yatokanayo na kodi, mapato yasiyotokana na kodi, mikopo ya ndani, mikopo ya nje na misaada ya wahisani. Hata hivyo, utekelezwaji wa bajeti iliyoidhinishwa ulikuwa kama ifuatavyo.

**Mapato**

Serikali iliweza kukusanya kiasi cha Sh. 25.31 trilioni sawa na asilimia 86 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, hivyo kuwepo na upungufu wa Sh. 4.24 trilioni sawa na asilimia 14. Hii inaonesha kushuka kwa uwezo wa Serikali kukusanya mapato kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo Serikali iliweza kukusanya asilimia 94 ya bajeti hivyo kuwepo na upungufu wa asilimia 6 tu.

Hali hii imesababishwa na makusanyo hafifu kutoka vyanzo viwili vya mapato. Kwanza, Serikali ilishindwa kukusanya asilimia 38.30 ya mapato yasiyotokana na kodi. Pili, Serikali ilishindwa kukusanya asilimia 46.55 kutoka mikopo na misaada ya nje ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa.


**Matumizi**

Katika mwaka 2016/17, Serikali ilitoa Sh. 23.79 trilioni kwa ajili ya matumizi, sawa na asilimia 81 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kama ilivyoripotiwa na CAG. Hii inaonesha kushuka kwa utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo Serikali ilitoa asilimia 89 ya bajeti iliyoidhinishwa. Hata hivyo, ukilinganisha mapato na matumizi kama yalivyoripotiwa na CAG, kuna tofauti ya Sh. 1.52 trilioni sawa na asilimia 4 ya makusanyo ambazo hazikuripotiwa matumizi yake au kutambuliwa kama bakaa. Aidha, Serikali kupitia Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa majibu Bungeni kuelezea namna tofauti hiyo ilivyojitokeza.


Sehemu kubwa iliyoathirika na utekelezaji huu wa bajeti ni miradi ya maendeleo ambapo Serikali ilitoa jumla ya asilimia 57 tu ya bajeti ya maendeleo katika mwaka 2016/17.

**Kielelezo Na. 3: Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2016/17**

## Mapato




## Matumizi



**Athari:** Kushuka kwa utekelezaji wa bajeti ya taifa kwa asilimia 14 ikilinganishwa na asilimia 6 za mwaka uliopita kulisababisha Serikali kushindwa kutekeleza sehemu kubwa ya miradi ya maendeleo. Aidha, hali hii iliathiri utoaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika ngazi za Halmashauri. Kama vile, Mamlaka za Serikali za Mitaa 167 hazikupatiwa Sh. 537.21 bilioni sawa na asilimia 51 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge. Kushindwa kukamilisha miradi ya maendeleo katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuliathiri moja kwa moja wananchi kwa kutopatiwa huduma bora kama vile afya, maji, elimu, miundombinu nk.

**Nini kifanyike:** Pamoja na mapendekezo ya CAG, WAJIBU inashauri serikali ipitie upya vyanzo vyake vya mapato ili iweze kuandaa bajeti inayotekelezeka. Aidha, Serikali iendelee kutekeleza mbinu ilizojiwekea za kupunguza matumizi ya kawaida ilikupata fedha nyingi zaidi za kutekeleza miradi ya maendeleo. WAJIBU inashauri, kwa kuwa majibu yaliyotolewa na Serikali Bungeni kuelezea tofauti ya Sh. 1.52 trilioni yalikuwa hayajakaguliwa na CAG, ni vema majibu hayo yakakaguliwa ili kuthibitisha usahihi wake.


### Jambo la 2: Changamoto Katika Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi

Kumekuwa nakushuka kwa uwezo wa serikali kukusanya mapato yake kama yalivyoidhinishwa kwenye bajeti ya mwaka 2016/17 ikilinganishwa na mwaka 2015/16 kutoka asilimia 94 hadi asilimia 86. Hali hii inaonyesha bado kuna udhaifu mkubwa katika udhibiti wa makusanyo ya ndani.

Ripoti ya CAG inaonesha udhaifu katika maeneo 7 yaliyosababisha Serikali kushindwa kukusanya kodi ya Sh. 7.63 trilioni ambayo ni sawa na asilimia 26 ya bajeti ya Taifa iliyoidhinishwa na Bunge. Maeneo haya ni kama yanavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 4 hapo chini:

**Kielelezo Na. 4: Maeneo yaliyosababisha Serikali kushindwa kukusanya Mapato ya kodi**

| | | Kiasi (Sh.Milioni) |
|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji wa Mitambo ya kuchenjua madini bila kuwepo kwa leseni hivyo kusababisha upotevu wa kodi | 231.66 |
| 2 | Mapato yasiyotokana na kodi ambayo hayakuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali | 14,546.47 |
| 3 | Kesi za muda mrefu katika Mamlaka za Rufaa za Kodi | 4,440,000.00 |
| 4 | Mifumo isiyoridhisha katika kushughulikia pingamizi za kodi | 2,862,450.00 |
| 5 | Mifumo ya udhibiti ya misamaha ya kodi ya mafuta kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji madini | 13,133.00 |
| 6 | Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizotoka katika maghala ya forodha | 29,500.00 |
| 7 | Usimamizi usioridhisha wa makusanyo ya madeni ya kodi | 271,657.14 |
| | **JUMLA** | **7,631,518.27** |




**Athari:** Hali hii imepelekea Serikali kushindwa kukusanya Sh. 7.63 trilioni ambazo kama zingekusanywa, mapato ya Serikali yangefikia Sh. 32.94 trilioni sawa na ongezeko la asilimia 12 zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa Serikali kushindwa kuteua makamu wenyeviti na wajumbe wa Bodi ya Rufaa na Baraza ya Rufaa za Kodi kumeipelekea Serikali kushindwa kukusanya Sh. 7.30 trilioni. Udhaifu katika kukusanya mapato, umeisababishia Serikali kushindwa kutekeleza sehemu kubwa ya mipango iliyojiwekea, hususani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo huduma za kijamii kama elimu, afya, maji na miundombinu zimekua ni tatizo kwa jamii katika shughuli zao za kujenga taifa.

**Nini kifanyike:** Serikali iimarishe utendaji na mifumo ya Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi katika kuendesha kesi za rufaa za kodi. Pia, kuhakikisha kuwa wakati wote nafasi za makamu wenyeviti na wajumbe wa taasisi hizi zinajazwa kulingana na sheria husika; jambo hili litaharakisha usikilizwaji wa kesi za rufaa za kodi ambazo zinazuia kiasi kikubwa cha mapato ya Serikali. Vilevile, ni muhimu sana kuziongezea uwezo wa kifedha taasisi hizi kwani bajeti zao ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu yao.

### Jambo la 3: Mapungufu Katika Usimamizi wa Deni la Taifa

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017, deni la taifa lilikuwa Sh. 46.08 trilioni ikiwa ni ongezeko la Sh. 5.04 trilioni sawa na asilimia 12 ikilinganishwa na deni la Sh. 41.04 trilioni lililoripotiwa na Serikali Juni 2016. Deni hili linahusisha; deni la ndani Sh. 13.34 trilioni na deni la nje Sh. 32.74 trilioni.

Katika ukaguzi uliofanyika mwaka 2016/17, CAG ameonesha kuwa deni la taifa linaendelea kukua kila mwaka kutokana na; mapato ya Serikali kuwa madogo ikilinganishwa na matumizi yake; ubadilishwaji wa hati za ukwasi kugharamia bajeti ya Serikali; ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo pamoja na hasara inayopatikana kutokana na kubadilisha fedha za kigeni kunakosababishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na fedha nyingine za kigeni.

Hata hivyo, ukaguzi wa CAG unaonesha mapungufu kadhaa katika usimamizi wa deni la taifa kama vile; kiasi cha Sh. 4.59 trilioni hakikuripotiwa kwenye deni la taifa hivyo kufanya ulipaji wake uwe mashakani. Kiasi hiki kinatokana na hela zilizokopwa kutoka kwenye mifuko ya pensheni kiasi cha Sh. 4.42 trilioni na dhamana zilizokiukwa masharti kiasi cha Sh. 166.64 billioni. Moja ya sababu za madeni haya kutojumuishwa kwenye jumla ya deni la taifa ni kukosekana kwa nyaraka za kuthibitisha madeni hayo.




**Athari:** Pamoja na kuwa deni la taifa ni himilivu kwa sasa, kumekuwa na ongezeko katika uwiano wa gharama za kulihudumia na mapato ya ndani kutoka asilimia 46 hadi kufikia asilimia 49 ikilinganishwa na matokeo ya ukaguzi wa mwaka 2015/16.

Kutokana na kutozingatiwa kwa ahadi ya Serikali katika ulipaji wa deni hili kwa mifuko ya pensheni, kunaweza kupelekea kuzorotesha utoaji huduma kwa wanachama wa mifuko hii.

**Nini Kifanyike:** Ingawaje ukubwa wa deni la taifa bado upo kwenye uwiano unaokubalika kwa kutumia vigezo vya Benki ya Dunia, pamoja na mapendekezo ya CAG, WAJIBU inashauri mambo yafuatayo yafanyike:

i. Ukopaji wa Serikali ulenge katika kuwekeza kwenye vitega uchumi vya nchi vitakavyochangia katika ukuaji wa haraka wa uchumi na kutengeneza nafasi za ajira nyingi katika kukabili tatizo la ajira lililopo nchini, hivyo kujenga uwezo wa serikali wa kulipa madeni yake.

ii. Mikopo inayokopwa ni kwa fedha za kigeni, na malipo yake huwa yanafanywa kwa fedha za kigeni. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuchunga thamani ya fedha yetu isishuke kwa kuwa Serikali itakuja kuhitaji fedha nyingi za ndani kulipia madeni ya nje.

iii. Mbali na kuwepo kwa vigezo vya kimataifa vya kupima uhimilivu wa deni la taifa, Serikali iangalie upya vigezo hivyo kwa kutilia maanani mzigo unaotokana na kuhudumia deni hilo.

iv. Ni wakati muafaka kwa taasisi zingine zisizo za kiserikali (AZAKI) kuanza kudai uwazi zaidi wa matumizi ya fedha za mikopo.

v. Bunge kama mwakilishi wa wananchi lidai ushirikishwaji zaidi kwenye mikopo mikubwa ya kitaifa.

### Jambo la 4: Rasilimali za Umma Zinavyoathiriwa na Udhaifu wa Udhibiti wa Mifumo ya Ndani

Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2016/17 imebainisha mapungufu katika udhibiti wa mifumo ya ndani ya usimamizi wa fedha na rasilimali za umma. Mapungufu haya yanatokana na;

i. Kuwepo kwa malipo ambayo hayakuwa na risiti za EFD yenye thamani ya Sh. 41.83 bilioni ikiwa ni ongezeko la Sh. 38.85 bilioni sawa na asilimia 93 ikilinganishwa na ripoti ya mwaka 2015/16.

ii. Faini zilizotokana na kucheleweshwa kwa malipo ya mikataba kiasi cha Sh. 587 milioni na malipo yaliyolipwa kwenye shughuli mbalimbali yenye thamani ya Sh. 487 milioni.

iii. Matumizi ya Sh. 397.23 bilioni yaliyofanyika nje ya bajeti iliyopitishwa. Kulingana na ripoti ya CAG, kuna baadhi ya taasisi zilizotumia zaidi ya fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti. Baadhi ya taasisi

hizi ni Idara ya Deni la Taifa na Idara ya Huduma za Kijamii kwa asilimia 101, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa asilimia 115, Tume ya Taifa ya Uchaguzi asilimia 192 na Idara ya Uhamiaji kwa asilimia 143.

iv. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya kulipa madeni ya miaka ya nyuma Sh. 219.47 bilioni. Ripoti ya CAG inaonesha kuwa kuna malipo yaliyofanyika ambayo hayakuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa. Hivyo, kutokana na malipo haya, serikali imeendelea kuzalisha madeni mengineyo na kusababisha kutotekelezeka kwa bajeti.

*(Chanzo: Ripoti ya CAG ya Serikali Kuu ya mwaka 2016/17, Uk. 35 - 40).*

**Athari:** Serikali kufanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ni uvunjaji wa Kifungu cha 19 cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa). Utaratibu huu ni mbovu na unapunguza uwezo wa bajeti iliyoidhinishwa kutumika kama ni nyenzo ya udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali.

Mapungufu yaliyoripotiwa ni jumla Sh. 659.60 bilioni, fedha hizi zingeweza kufidia kiasi cha Sh. 532.21 bilioni ambacho hakikutolewa katika utekelezaji miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa 167 zilizoripotiwa.


**Nini kifanyike:** Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 imeweka wazi utaratibu wa kufuatwa kuhusu malipo yanayofanywa nje ya bajeti iliyoidhinishwa. Malipo yote yaliyofanywa zaidi ya kilichokuwa kimeidhinishwa au malipo ambayo hayakuidhinishwa na Bunge sharti Serikali iandae bajeti ya ziada na kuiombea kibali cha Bunge. Pia, TAMISEMI ihakikishe Halmashauri zote zinatumia kikamilifu mfumo wa Epicor ili uwezeshe udhibiti wa matumizi kulingana na bajeti.

### Jambo la 5: Madhara ya Uhaba wa Watumishi

Uhaba wa watumishi katika taasisi za serikali bado umeendelea kuwa tatizo. Hii nikutokana na ongezeko la nafasi zilizowazi kufikia 34,081 ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi 54,937 kwa taasisi 48 zilizofanyiwa sampuli katika ripoti ya CAG ya mwaka 2016/17. Upungufu huu ni sawa na asilimia 62 ikilinganishwa na uhitaji wa watumishi wanaohitajika. Kwenye ripoti ya CAG ya mwaka 2015/16, taasisi 38 zilizochukuliwa kama sampuli zilikuwa na nafasi 11,892 zilizokuwa wazi.

Tatizo hili limejitokeza kwa kiasi kikubwa katika Sekretarieti za Mikoa, Mahakama na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 5 hapo chini. *(Chanzo: Ripoti ya CAG ya Serikali Kuu ya mwaka 2016/17, Uk. 135)*

### Kielelezo Na. 5: Taasisi za Serikali Kuu Zinazoongoza kwa Uhaba wa Watumishi



**Athari:** Ni ukweli usiofichika kuwa upungufu wa watumishi wa umma unaathiri ufanisi wa utendaji kazi wa sekta hiyo. Vilevile, upungufu unaoripotiwa na CAG unachangia kutokukamilika kwa miradi na uzoroteshaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Nini Kifanyike:** Serikali ifanye tathmini iliyo sahihi ya uhitaji wa watumishi, kwani kuwa na upungufu wa asilimia 62 ya watumishi na bado Serikali iweze kujiendesha kwa ufanisi unaotegemewa ni kitu ambacho hakiwezekani. Vilevile, Bunge lisisitize Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kufanya tathimini ya kina ya mahitaji ya watumishi wa umma na kuandaa mpango wa kuajiri ili kukidhi mahitaji yatakayobainiwa.

### Jambo la 6: Wakala wa Serikali Bado ni Tegemezi kwa Serikali Kuu

Sheria Na. 30 ya mwaka 1997, inayosimamia Wakala za Serikali inazitaka Wakala zote kufanya kazi zao kwa mujibu wa kanuni za biashara na kuhakikisha kuwa, mapato yao yanatosheleza kulipia matumizi yao na ziada kupelekwa Mfuko Mkuu.

Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza katika usimamizi wa rasilimali za Wakala wa Serikali:


i. Wakala bado zinaitegemea Serikali Kuu kwa asilimia 82 ya bajeti zake. Utegemezi huu umeongezeka kutoka asilimia 55 iliyokuwa mwaka 2015/16.

ii. Kutotolewa kwa Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa kiasi cha Sh. 854.06 bilioni sawa na asilimia 57 ya bajeti ya maendeleo ya Wakala 33 zilizokaguliwa mwaka 2016/17.

iii. Maendeleo sekta ya Maji: Kulingana na ripoti ya Ukaguzi, inaonesha kuwa Bodi za Mabonde ya Maji kupitia Mradi wa Maendeleo Sekta ya Maji zilipokea asilimia 13 tu ya bajeti iliyoidhinishwa.

iv. Malipo zaidi yaliyotolewa kwa wakandarasi kutokana na marekebisho ya bei katika mikataba ya ujenzi wa barabara Sh. 1.18 bilioni. Kiasi hicho kililipwa kimakosa kwa wakandarasi kutokana na mapungufu katika kutumia kanuni za kukokotoa kiasi cha malipo kinachotokana na mabadiliko ya bei.

*(Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi Serikali Kuu 2016/17,Uk. 141 - 157)*




**Athari:** Utegemezi wa Wakala za Serikali kwa Serikali Kuu wa asilimia 82 ni mzigo mkubwa kwa Serikali ambao haukutarajiwa. Athari ya tatizo hili ni matumizi ya fedha za Serikali katika kuendesha Wakala hizi, fedha ambazo zingeweza kutumika kulipia miradi ya maendeleo katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazogusa maisha ya wananchi. Siyo siri kuwa, taifa bado linakabiliwa na changamoto nyingi za wananchi kupata maji safi na salama, huduma za afya na nyinginezo. Aidha, itakuwa ni ndoto kwa Serikali kuweza kutatua tatizo la upatikanaji wa maji kama Mabonde ya Maji nchini yanapewa asilimia 13 tu ya fedha zinazohitajika za maendeleo.

**Nini Kifanyike:** Serikali iwe makini zaidi katika kuanzisha wakala mpya. Ni vizuri Serikali ikawa inafanya uchambuzi wa kina (feasibility study) kabla ya kuanzishwa kwa Wakala za Serikali ili kujipunguzia mzigo wa kulipia gharama za uendeshaji wao.

Serikali ifanye uchambuzi wa Wakala zilizopo kuona umuhimu wa kiuchumi na katika utoaji wa huduma wa Wakala hizi; zile ambazo zitaonekana hazina umuhimu mkubwa majukumu yake yaunganishwe na Wakala nyingine au Taasisi nyingine za Serikali.

### Jambo la 7: Vyama vya Siasa Kutozingatia Sheria za Fedha

Sheria na taratibu zinawekwa ili kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa fedha na rasilimali ndani ya vyama husika. Ripoti ya CAG ya mwaka 2016/17, inaonesha kuwa Hati Mbaya zote 7 zilitolewa kwa vyama vya siasa. Pia, kumekua na mapungufu mbalimbali katika utaratibu wa udhibiti na usimamizi wa fedha za vyama vya siasa. Baadhi ya Mapungufu hayo ni kama yafuatayo:

i. Kumekuwa na mikopo ambayo haikuthibitishwa mapokezi yake ndani ya vyama yenye thamani ya Sh. 2 bilioni.

ii. Makusanyo ya fedha za vyama ambayo hayakupelekwa benki Sh. 2.3 bilioni

iii. Manunuzi yaliyofanyika na vyama vya siasa bila kushindanisha wazabuni Sh. 2.13 bilioni

iv. Vyama vya siasa kutokuwa na rejista za mali za kudumu

v. Malipo yaliyofanyika na vyama vya siasa yenye nyaraka pungufu ya thamani ya sh. 735.98 milioni

vi. Kutokurejeshwa kwa masurufu yaliyochukuliwa kwenye vyama vya siasa yenye thamani ya Sh. 558.92 milioni

vii. Mikopo iliyotolewa na vyama vya siasa isiyo na faida yenye thamani ya Sh. 12.01 bilioni

viii. Mikopo ya uwekezaji iliyotolewa na vyama vya siasa bila kuzingatia taratibu na kutokuwepo na viambatisho yenye thamani ya Sh. 455.97 milioni.

**Athari:** Vyama vya siasa madhumuni yake ni kushika dola, hivyo chama cha siasa kupata hati mbaya ya ukaguzi ni ishara ya kutokuwa na uwezo wa kuongoza dola.




**Nini kifanyike:** Msajili wa vyama vya siasa anashauriwa kuviwajibisha vyama vya siasa ambavyo vitapata hati mbaya kwa mara tatu mfululizo.

# Sehemu ya Nne

## Hitimisho

WAJIBU inatarajia kupitia ripoti hii itawakumbusha Maafisa Masuuli na wahusika wengine wote kuhusu mapendekezo ya CAG na umuhimu wa utekelezaji wake. Vilevile, WAJIBU inatarajia ripoti hii itaongeza uelewa wa wananchi juu ya ripoti ya CAG ya Serikali Kuu ya mwaka 2016/17.

Aidha, WAJIBU inatarajia ripoti hii itawawezesha wananchi kupitia Asasi za Kiraia (AZAKI) na wawakilishi wa wananchi kudai uwajibikaji kutoka kwa wenye mamlaka (duty bearers) pale watakapoona hawajawajibika ipasavyo.

Ripoti hii itachangia kufanya mapendekezo ya CAG yawe na uhai wa muda mrefu zaidi kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita, hivyo kuwepo na matarajio ya ongezeko la utekelezaji wa mapendekezo hayo.

**WAJIBU - Institute of Public Accountability**
P. O. Box 13486 Dar Es Salaam
Barua pepe: admin@wajibu.or.tz ; Simu: +255 22 266 6916
Tovuti: www.wajibu.or.tz